

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

Biografia ya Profesa / Mohammed Mukhtar Juma

Waziri wa Wakfu wa Misri na Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu

Mwanachama wa jopo la utafiti na Mwenyekiti wa Ukumbi wa Usamehevu na Usawa

Mheshimiwa Profesa Mohammed Mukhtar Juma amemaliza masomo ya chuo katika kitivo cha masomo ya Kiislamu na lugha ya kiarabu katika Chuo Kikuu cha Al Azhar Sharif – Kairo, kwa maksi za juu kabisa na alikuwa ameshika nafasi ya kwanza katika mwaka wa mwisho wa kitivo. Kisha akapata shahada ya uzamili (MA) katika masomo ya lugha ya kiarabu na fasihi yake kwa kiwango (maksi) za juu kabisa (Excellent). Kisha baada ya hapo akapata shahada ya uzamivu (PHD) kwa maksi za juu zaidi na heshima ya kwanza(first honor).

Akachaguliwa kufanya kazi katika kitivo chake cha Al azhar ya kuwa, kisha akawa mwalimu msaidizi, akawa mhadhiri, kisha mhadhiri msaidizi (associate professor), kisha mhadhiri mkuu (professor), na kupandishwa cheo na kuwa Makamu wa kitivo, kisha akawa mkurugenzi wa Kitivo cha masomo ya Kiislamu na Kiarabu kwa wavulana – Kairo. Pamoja na kuwa ni Mkuu wa chuo, akachaguliwa kuwa ni mwanachama katika ofisi ya ufundi ya Mkuu wa Chuo cha Al azhar katika Mambo ya ulinganiaji na utangazaji wa dini. Kisha akachaguliwa kuwa ni Waziri wa Wakfu wakati wa uongozi wa Pro. Hazim Al–Beblawiy tarehe 16 July 2013. Na kutokana na juhudi zake kubwa na huduma nyingi za kuuhudumia uislamu na kuirudisha Misri

katika ukale wake wa Azhar isiyokuwa na misimamo mikali akachaguliwa katika vipindi viwili (muhula miwili) vya uongozi wa serikali ya Mhandisi Ibrahim Mahlab, muhula wa kwanza na wa pili.

Pia akachaguliwa kuwa ni mwanachama wa jopo la watafiti wa kiislamu. Na Baraza la Muungano la kimataifa la wanachuo waliomaliza Al Azhar Sharif. Na vilevile akachaguliwa kuwa ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wakfu wa Kiarabu na Mwenyekiti wa ukumbi wa baraza la usamehevu na usawa katika Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu kwa kupata ridhaa ya wahadhiri wasaidizi na wahadhiri wakuu (kupendekezwa. Na pia akawa Mwenyekiti wa ujumbe wa Mahujaji wa Kimisri kwa muda wa miaka mitatu mfululizo. Pia alichaguliwa kuwa ni balozi wa usamehevu na amani mnamo mwaka 2015 kupitia taasisi ya Usamehevu na amani ya nchini Kuwait.

Na kutokana na juhuzi zake nzuri katika Nyanja za masomo ya fasihi na uhakiki na masomo ya kurani akachaguliwa kuwa ni mwanachama katika taasisi mbali mbali za kisayansi na za kifasihi, pamoja na kuwa ni mwenyekiti wa Baraza Kuu la mambo ya kiislamu pia ni mwanachama wa umoja wa waandishi wa Misri na Umoja wa waandishi wa Kiarabu, na jumuiya ya wanafasihi wa kimataifa wa kiislamu. Na ni mwanachama wa kamati ya hukumu ya wanachama wa chuo kikuu kwa kupata daraja za juu katika chuo cha Al azhar katika nyanja za fasihi na uhakiki. Ameshiriki katika mikutano na semina nyingi za kisayansi na za kifasihi ndani ya Misri na nje pia, na katika mikutano na semina nyingi aliwahi kuwa ni Mwenyekiti wa vikao hivyo. Na vile vile ni msimamizi wa wanafunzi wa madarasa ya juu (MA) na (PHD) juu ya tafiti zao na pia kuhakiki nyaraka nyingi za kielimu na baadhi ya

magazeti ya kielimu na aliwahi pia kuwa ni mhariri wa baadhi ya magazeti. Na alishiriki katika kuweka mitaala ya kielimu ya chuo cha Al Azhar – Kairo. Na katika vitivo vya malezi nchini Oman.

Anasaidia sana katika Nyanja za vyombo vya habari vya kusikika na vya kusomwa ndani ya Misri na nje yake. Na ana tafiti nyingi na ametunga vitabu vingi vya kuelimisha, mfano; “kuelekea kusawazisha hotuba za dini”, “makala katika dini na maisha” na kitabu hiki kimefasiriwa kwa lugha kumi na tatu, “anga la elimu”, nacho kimefasiriwa kwa lugha saba. “chakula cha akili”, “kutengua mawazo ya msimamo mkali”, “katika siri za kauli za Kurani”, “kuishi kwa salama na kushirikiana kati ya dini” “kuelekea katika marekebisho”, “usawa wa kilugha”: utafiti wa kisayansi ndani ya aya za Kurani, “hoja ya aya na athari zake kupitia maneno ya kifasihi”, utafiti wa kielimu kwa mtazamo wa Kurani Tukufu. Na “uadilifu kati ya wanakale na watu wa kisasa”, :uhakiki, na “ mjadala kuhusu uwepo na kutokuwepo kati ya wanakale na watu wa kisasa”. Na ana zaidi ya vitabu ishirini. Kama ambavyo amechangia sana katika kuhakiki na kukitoa kitabu cha “muongozo wa mwalimu katika maadili na tabia na uzalendo” ambacho kimeandaliwa na Wizara ya Malezi na Elimu ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, akaweka utangulizi wa kimalezi, pamoja na hayo yote ana pia makala ya kila wiki katika magazeti muhimu ya nchini Misri.